



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA KUHUSU MATUMIZI YA SIMU NDOGO YA MKONONI  
KWENYE UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA

Kigoma, 18 Julai, 2024

Katika vikao vya Tume na Wadau mbalimbali, walitoa maoni na ushauri kwa Tume ili ione uwezekano wa watumiaji wa aina zote za simu ikiwemo simu za kawaida (maarufu kitochi au kiswaswadu) na ambao wamo kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, wawe na uwezo wa kuanzisha mchakato wa kuboresha taarifa au kuhamisha taarifa zao.

Tume imefanya kazi maoni na ushauri huo na kuanzia tarehe 20 Julai, 2024 watu wote wenyе simu za kawaida (maarufu kama kitochi au kiswaswadu) na watahitaji kuboresha ua kuhamisha taarifa zao, watapata huduma hiyo kwa kupiga USSD Code \*152\*00# na kubonyeza namba 9 kisha kuendelea na hatua zingine kama itakavyokuwa inaelekezwa kwenye simu husika.

Mpiga kura anayetumia njia hii atapokea namba maalum (token) kupitia simu yake kisha atalazimika kwenda na namba hizo kwenye kituo anachotarajia kutumia kupiga kura kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 ili kukamilisha mchakato na kupewa kadi mpya.

**KUJIANDIKISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA!**

Imetolewa na:

Kailima R. K.

**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**